

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA KUMI NA MBILI

19 APRILI, 2021



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA KUMI NA MBILI – TAREHE 19 APRILI, 2021

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Rais (TAMISEMI) kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Rais (TAMISEMI) kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

III. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

94. MHESHIMIWA KATANI AHMAD KATANI (TANDAHIMBA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itaunga mkono juhudi za Wananchi wa Kata za Mnyawa, Nanhyanga, Nambahu, Kitama na Nguja ambao wameanza kujenga Vituo vya Afya kwa nguvu zao wenyewe kwa kutoa fedha ili kukamilisha ujenzi wa Vituo hivyo.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

95. MHESHIMIWA HAJI MAKAME MLENGE (CHWAKA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, ni lini Warithi wa Askari E.2152 (Makame Haji Kheir) aliyefariki tangu Mwaka 2003 akiwa Mtumishi wa Jeshi la Polisi Kituo cha Madema watapewa mafao yake.

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII,
JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**

**96. MHESHIMIWA JANETH ELIAS
MAHAWANGA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya,
Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na
Watoto:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia
Wajasiriamali wadogo kupata bima ya afya
kupitia utaratibu wa vikundi ambao ulikuwa
msaada mkubwa sana kwenye Jamii.

**97. MHESHIMIWA MARTHA NEHEMIA GWAU
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya,
Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na
Watoto:-

Je, ni kiasi gani cha Zebaki kinaingizwa nchini
kila Mwaka.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

**98. MHESHIMIWA TECLA MOHAMED UNGELE
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu,
Sayansi na Teknolojia:-

Je, Serikali haioni haja kukipandisha hadhi Chuo cha Ualimu Nachingwea kuwa Chuo Kikuu cha Ualimu kutokana na mahitaji ya Walimu kuwa makubwa.

WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

99. MHESHIMIWA STELLA SIMON FIYAO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itatengeneza kwa kiwango cha lami barabara ya kutoka Mbalizi – Mkwajuni ili kuepusha adha wanayokutana nayo Wananchi hususani kipindi cha mvua.

100. MHESHIMIWA HAMIS MOHAMED MWINJUMA (MUHEZA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:- Kasi ya ujenzi wa barabara ya Muheza – Amani sio ya kuridhisha na hadi sasa maeneo korofi bado hayajafikiwa:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwa na awamu ya pili katika ujenzi wa barabara hiyo kuanzia Amani kuelekea Muheza ili kutatua changamoto zilizopo wakati ujenzi wa barabara ukiendelea.

101. MHESHIMIWA DEUS CLEMENT SANGU (KWELA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya kilomita 200 kutoka Kilyamatundu kupitia Ilemba, Muze, Mfinga mpaka Majimoto.

WIZARA YA NISHATI:

102. MHESHIMIWA RIDHIWANI JAKAYA KIKWETE (CHALINZE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, ni lini Serikali itawalipa fidia Wananchi wa Chalinze waliopisha ujenzi wa miundombinu ya miradi ya kusafirisha umeme kutoka Kinyerezi na Bwawa la Mwalimu Nyerere.

WIZARA YA MAJI:

103. MHESHIMIWA ZACHARIA PAULO ISSAAY (MBULU MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Wakala wa Maji Vijijini atachimba visima sita katika Vijiji vya Aicho, Gidamba,

Gunyoda, Silaloda, Boboa na Titiwi katika Jimbo la Mbulu Mjini.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais (TAMISEMI) kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

DODOMA
19 APRILI, 2021

S. KAGAIGAI
KATIBU WA BUNGE